BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Ishirini – Tarehe 06 Juni, 2023**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka 2023/2024.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa Mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

159. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Katika majukumu makubwa ya Wizara yako ni pamoja na kutunza mazingira na kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi, ili kuhakikisha wananchi wetu wanaishi kwa usalama.

(a) Je, ni taasisi gani kutoka nje ambazo zinaisaidia nchi yetu katika suala la kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

(b) Je, ni taasisi zipi binafsi za ndani ya nchi zinazotekeleza ajenda ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

(c) Ni maeneo gani ambayo yameathiriwa zaidi na mabadiliko haya ya tabianchi na jitihada zipi zinafanyika kuinusuru hali hiyo.

**<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>**

79. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuchukua uamuzi wa kuvikodisha baadhi ya visiwa vyake Unguja na Pemba, kikiwemo kisiwa cha Kunjwi kilichopo shehia ya Mtangani. Hata hivyo, kulikuwa na wananchi wengi waliokuwa wanakitumia kisiwa hicho kwa kilimo, lakini hadi leo hii hawajalipwa thamani ya mazao yao waliyokuwa wakulima katika kisiwa hicho.

(a) Je, Wizara yako ina taarifa yoyote ya suala hili.

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wakulima hao.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

120. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali inastahili kupongezwa na kupewa shukrani kwa juhudi zake za kuitengeneza barabara kongwe ya Chake Chake-Wete kupitia Mzambarauni (Mzambarau Takao). Hata hivyo, zoezi hilo limeliathiri soko la mji huo.

(a) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kulirejesha soko hilo bila ya kuathiri makaazi ya wananchi wa mji huo.

(b) Je, ni lini na kwa viwango gani soko hilo litajengwa na kwa gharama zipi.

(c) Katika maeneo ya soko la zamani kuna eneo kubwa nyuma yake, Je, Serikali haioni ulazima wa kulirejesha soko hilo katika maeneo ya nyuma ya soko la zamani ili kuepuka usumbufu kwa wananchi na makaazi yao.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

143. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Masomo ya udereva yamesaidia sana kupunguza ajali barabarani, huku kukiongezeka taaluma sahihi ya utumiaji wa vyombo vya moto hapa nchini.

(a) Je, kuna umuhimu gani wa kuwafundisha wanafunzi wanaosomea udereva kwa kutumia gari zenye mfumo wa kizamani ambazo nyingi zao kwa sasa hazionekani kuwa na soko.

(b) Je, Wizara yako haioni kuwa ipo haja ya kuweka uhuru kwa mteja au mwanafunzi kufundishwa kwa aina ya gari anayoitaka mwenyewe kwa mujibu wa matumizi yake ili kuondoa malalamiko haya.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

187. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na wimbi kubwa la wanafunzi wanaofanya vibaya sana katika mitihani ya kidato cha nne hapa Zanzibar, jambo ambalo halitoi taswira nzuri kwa nchi yetu.

(a) Je, Serikali zetu mbili zinalichukulia vipi jambo hili.

(b) Je, ni upi mkakati hasa wa Serikali wa kukabiliana na hali hii kwa muda mfupi na kwa muda mrefu.

(c) Je, Serikali ina mpango gani kwa watoto wengi walioko mitaani na ambao wameanguka katika mitihani ya kidato cha nne na wamekwama kimaisha.

**Wizara ya Afya:**

114. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na masikitiko kwamba tokea Disemba 2022, baadhi ya huduma zilizotarajiwa kutolewa na taasisi binafsi (outsourced) kama zilivyopangwa na Serikali, zimekuwa zikisuasua katika upatikanaji wake zikiwemo huduma za uchunguzi zitolewazo na kitengo husika cha 'diagnostic unit'.

(a) Je, ni huduma zipi hadi sasa zinazotolewa na taasisi

binafsi kwa niaba ya Serikali katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja.

(b) Je, ni upi utaratibu wa kuzipatia huduma kama hizo hospitali zote kumi za Wilaya na moja ya Mkoa.

(c) Je, kwa vile suala la afya si la kusubirishwa sana, ni ipi tathimini ya Serikali na wadau wa afya Zanzibar, kuhusiana na huduma hizo zinazotolewa na taasisi binafsi.

<u>**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**</u>

222. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kwa muda mrefu sana Zanzibar kumekuwa na changamoto ya ujenzi holela wa nyumba za makaazi usiozingatia mipango miji hasa katika maeneo ya miji mipya. Lakini pia hata baadhi ya ujenzi wa nyumba za makaazi zinazofanyiwa ukarabati mpya katika jiji la Zanzibar umekuwa hauvutii na hauendani na viwango vya ukuwaji na uwekaji wa mandhari nzuri ya jiji.

(a) Je, Serikali inayo sera ya majenzi inayoweka vigezo vya majengo ya makaazi ya watu yajengwe kwa utaratibu upi katika kila eneo lililopangwa kwa ajili ya makaazi ya watu.

(b) Je, kwa nyumba zinazojengwa kando au karibu na barabara kuu, Serikali haioni haja ya kuweka masharti ya lazima kuwa ujenzi wa nyumba kama hizo ziwe za ghorofa ili mandhari ya jiji la Zanzibar na viunga vyake yawe bora zaidi.

(c) Je, Serikali inayo ramani ya miaka 50 ijayo ya mipango miji ya kuonesha jiji la Zanzibar na viunga vyake linatakiwa liweje na mpango wa kuitekeleza upoje.

<u>**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**</u>

228. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Sera ya Serikali ya kuelekea uchumi wa buluu wenye tija kwa wote inatia matumaini. Hata hivyo, kukosekana kwa baadhi ya miongozo na zana za kuutekeleza, kunatia mashaka juu ya mafanikio yake ya haraka.

(a) Je, Serikali imefikia wapi katika kuwa na sheria na mpango mkakati wa uzalishaji, uhifadhi, matumizi ya uvuvi wa mwambao na bahari kuu.

(b) Je, Serikali kwa ujumla wake imewekeza kiasi gani katika uvuvi wa bahari kuu kwa kipindi cha mwaka 2020-2023.

(c) Ili kuvutia wawekezaji katika uchumi wa buluu, Serikali imefikia wapi katika kuboresha miundombinu ya sekta ya uvuvi wa bahari kuu ikiwemo mfumo wa kodi, upatikanaji wa mafuta kirahisi, bandari yenye ufanisi, nyenzo bora za usimamizi, ukarabati, uangalizi, na uendeshaji wa vyombo vinavyotumika bahari kuu.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

241. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kuwa maeneo mengi ya kisiwa cha Pemba yamekuwa na ukosefu mkubwa wa maji safi na salama. Na kwa kuwa pamoja na jitihada kubwa inayofanywa na Wizara hadi leo hii bado suluhisho la tatizo hilo halijapatikana.

Je, ni lini Serikali itaanzisha utaratibu wa kuvuna maji ya mvua na kuyahifadhi kwenye mabwawa sambamba na kuyatumia maji ya bahari kwa ajili ya kuzalisha maji safi hasa kwa matumizi ya nyumbani kama wanavyotumia baadhi ya nchi nyengine duniani.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka 2023/2024.

Zanzibar,
06 Juni, 2023.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA